REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THIRD ASSEMBLY-SECOND SESSION

THE HANSARD

Monday, 25th March 2024

The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2:30 p.m.

[The Speaker (Hon. Mwambire) in the Chair]

PRAYER

PAPERS LAID

KILIFI COUNTY POLICY FOR COOPERATIVE DEVELOPMENT

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Tete.

Hon. Tete: Thank you, Mr. Speaker. Sir. I wish to lay on the Table of this House the Kilifi County Policy for Cooperative Development. Thank you.

(Hon. Tete laid the document on the Table)

REPORT ON THE SECTORAL COMMITTEE OF GENDER CULTURE, SOCIAL SERVICES, AND SPORTS ON GENDER-BASED VIOLENCE POLICY

The Speaker (Hon. Mwambire): Okay, you'll share with the Clerk. Next one, Chairperson, Gender, Culture, Social Services and Sports Committee.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you, Mr. Speaker. I also wish to lay on the Table of this House a Report of the Sectoral Committee on Gender, Culture, Social Services, and Sports on the Gender-Based Violence Policy. Thank you.

(Hon. (Ms.) Sidi laid the document on the Table)

STATEMENTS

ORDER OF BUSINESS FOR THE WEEK COMMENCING 25TH MARCH 2024

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Rose Baraka.

Hon. (Ms.) Rose: Thank you, Mr. Speaker. Sir. I wish to lay down the programme of the County Assembly Business. On Monday, 25th March 2024 we have: -

The tabling of the Kilifi County Policy for Cooperative Development; Motion on the Resumption of debate on Governor's Second Address, Third Assembly 2024; Notice of Motion on Capitation Grant of Vocational Training Centres; Adoption of the Report of the Sectoral Committee on Gender, Culture, Social Service and Sports on the Gender-Based Violence Policy; Statement sought by Hon. Benson Ngirani from the Department of Education and ICT regarding Mulungu wa Mawe and Rare ECDE Centres; Statement, sought by Hon. Benson Ngirani from the Department of Health and Sanitation Services regarding Sokoke Dispensary; Statement sought by Hon. Benson Ngirani from the Department of Trade, Tourism and Cooperative Development regarding Wezesha Fund Status.

On Tuesday, March 26th, 2024, at 2:30 p.m. we have: -

Tabling of Report of the County Public Investments and Accounts Committee on the consideration of the Reports of the Auditor General on the financial statements of Kilifi County Executive for the financial year ending 30th June 2021.

Notice of Motion on the adoption of Report of the County Public Investments and Accounts Committee on the consideration of the Report of the Auditor General on the Financial Statements of the Kilifi County Executive for the financial year ending 30th June 2021.

A statement sought by Hon. Brown Safari Kahindi from the Department of Health and Sanitation Services regarding Tunzanani Dispensary.

On Wednesday, March 27th, 2024, at 2:30 p.m. we have: -

Notice of Motion for the Hardship Allowance of ECDE teachers in Kilifi County. Statement sought by hon. Edward Ziro from the Department of Education and ICT regarding Hademu ECDE and Hademu Vocational Training Centre.

A Statement sought by Hon. Naphtali Kombo Nyae from the Department of Education and ICT regarding the supply of training equipment in the County Vocational Training Centers.

A Motion on Capitation Grants for Vocational Training Centres; A Motion on the Adoption of the Report of the Sectoral Committee on Gender, Culture, Social Services and Sports on the Gender Based Violence Policy.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

MOTION

GOVERNOR'S SECOND ADDRESS TO THE THIRD ASSEMBLY

THAT, the Thanks of the County Assembly be recorded for the exposition of Public Policy contained in the Second Address of the Governor His Excellency Gideon Maitha Mung'aro, OGW delivered on Wednesday, 13th March 2024.

(Hon Tete on 19.05.2024)

(Resumption of Debate interrupted on 19.05.2024)

The Speaker (Hon. Mwambire): Yes, Members, it is about the resumption of the debate of the Governor's Second Address, Third Assembly for those Members who did not get an opportunity to speak on the same in the previous occasions or sittings. Okay, so you can now make your request so that you can also ventilate. Like the last time, I'm worried when we're dealing with this issue and then …Okay, I'm not seeing Members make requests. Okay. Hon. Mohamed.

Hon. Mohamed: Asante, Bw. Spika, kwa kuweza kunipatia fursa hii. Wacha nigeuze kwa lugha ya Kiswahili ili wale wana Bamba waweze kusikia kile ambacho… Nataka kuchukua fursa hii kuweza kupeana shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kuweza kutufikisha hapa leo na pia nisema *saumu makbul* kwa Waislamu wote ambao wako na saumu maanake naona kanzu zimevaliwa lakini wengine saumu hazipo, kwa wale ambao saumu zipo, *saumu makbul.*

The Speaker (Hon. Mwambire): Nafikiri wako akina mheshimiwa Ngirani, Tete, Thaura, Mkadi, Rafiki, Ray wengi sana ambao wamejumuika na nyinyi kwa hivyo endelea mheshimiwa Mohamed.

Hon. Mohamed: Wanasema nisiwatenge, Waisilamu wote, *saumu makbul* ambao wako kwa Bunge hii tukufu.

Mimi pia niungane na wenzangu katika kupeana shukrani na pia kuweza kumpatia Gavana wetu kongole kwa hotuba yake ambayo aliweza kutoa hapa Bungeni. Kwa machache, niweze pia kupeana changamoto kwa wale ambao wameweza kupewa nafasi hizi za kuweza kufanya kazi pamoja na mstahiki Gavana. Kwanza nipeane kongole zangu kwake kwa sababu mstahiki ana bidii ya kutafutia gatuzi hili la Kilifi mazuri. Lakini pia niseme ya kwamba ipo haja ya kila mstahiki akipata nafasi ya kutoka nje na kutafuta wafadhili ili watusaidie hapa Kilifi. Kile kitengo kilichoundwa, kwamba kinasimamia wafadhili na sekta ya kibinafsi iwe kinaweza kutimiza na kuona kwamba wanamkumbusha mstahiki kwa yale yote anaenda kututafutia na kuingia katika mikataba na wafadhili tofauti tofauti.

Tumeona Gavana ameelekea nchi za ughaibuni ili kututafutia na kuingia mikataba na wahisani tofauti tofauti, lakini utekelezaji wake umekuwa wa pole pole mno. Ninatoa mfano. Kule Bamba kuna wahisani ambao walikuja na tukawapeleka kwa Gavana na kukubaliana safari ya kwenda nje ikafika Gavana akaenda, wakaweka saini makubaliano lakini hadi leo yale tuliyokubaliana na wahisani bado hatujafanya.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kuna stahili kuchimbwa mabwawa kule Bamba, na kwa upande wetu ni kupeana mashini za kuchimba yale mabwawa; ukiangalia mbali na kwamba kulikuwa na mvua nyingi ilinyesha lakini hadi leo ile ahadi tuliyoweka kama Kilifi Kaunti hatujatimiza. Hivi basi itakuwa vyema kwa kitengo kilichobuniwa na Gavana kuangalia mikataba yote tuliyoingia na wahisani inukuliwe na kufwatiliziwa ili tuone manufaa na maono ya Gavana kutimia.

Pia, nimpe kongole Gavana kwa kuwa akiona mambo hayaendi sawa basi kwa haraka huunda tume na tume hiyo huchunguza na kutupa ufafanuzi wa hilo jambo. Nikitoa mfano wa hivi karibuni katika hotuba yake hapa alitueleza kuwa kulikuwa na shida katika sekta ya *Supply Chain*; aliunda tume ambayo ilichukua malalamishi na kuona kwamba baadhi ya wafanyaji kazi ambao wako pale na hawafanyi kazi vyema waliwekwa nje kwa muda na hiyo ilituathiri kama wana Kilifi kwa sababu utendajikazi wetu ulichelewa na mambo yalienda pole pole. Tume ilifanya uchunguzi wake na kuna baadhi walirudishwa kazini na wengine bado.

Hili Bunge linafaa kupata Ripoti ya Tume kama hizi tukiingia hapa baada ya kuchaguliwa kule nyanjani. Gavana aliunda tume tatu. Kulikuwa na tume ya kuangazia jinsi ya utendakazi wa *Public Service*, kulikuwa na tume ya *Pending Bills* na mpaka leo hatujapata Ripoti hizo. Tunajua Gavana alikabidhiwa Ripoti hizo na ni muhimu Bunge hili lijue kwa sababu ni pesa za umma zilizotumika kulipa wale wanakamati waliokuwa pale kwa hivyo ni vyema pia, kupitia kwa kiongozi wa walio wengi Bungeni tupate Ripoti zile. Pia, ikiwezekana, tujue wale wafanyaji kazi waliowekwa kando walipatikana na makosa gani.

Nataka kumpa kongole kwa hotuba yake kwa sababu, wakati tukiingia kulikuwa na lalama kuwa *casual workers* walikuwa hawajalipwa kwa muda mrefu lakini alilichukua kama jukumu na akafanya bidiii wote wakalipwa. Kuna mipangilio kuwa *casual workers* wachukuliwe na wawe wafanyaji kazi wa kudumu katika serikali ya Kaunti lakini mpaka sasa hatujajua kinachoendelea. Ingekuwa vyema kama Bunge tungejuzwa imefikia wapi na wanaendelea vipi. Kulingana na Gavana, *casuals* wote wamelipwa lakini ukweli ni kwamba baadhi yao wanaofanya katika zahanati zetu hawajalipwa pesa zao. Ni vyema tukipata Ripoti hizo tujue ni vipi swala hili lilivyoshughulikiwa.

Tulipoingia katika Bunge hili, kulikuwa na shida katika tume ya uajiri wa Kilifi na kwa kauli mmoja tulikubaliana na tukabandua tume iliyokuwa na tukaweza kuweka tume mpya. Jambo hili lilirudisha matumaini ya vijana wengi. Kama tunavyojua, gatuzi letu la Kilifi halijawahi ajiri lakini wakati tulibandua ile tume na kuweka tume nyingine, ilirudisha matumaini mengi sana kwa wakaazi wa Kilifi.

Natoa kama changamoto tume tuliiweka na hadi sasa bado iko na nafasi mbili ambazo hazijajazwa; hizo nafasi zifaa zijazwe. Tuna tetesi kuwa ile tume iliyotoka kuna wakati ilihudumu na maafisa kidogo. Kwa hivyo, tusipeane nafasi tena kwa hii nayo iendelee kuhudumu na wanachama nusu. Hata Gavana aliona hilo na kusema karibuni atajaza. Ombi tu kwa Gavana, kuna baadhi ya sehemu ambazo hazijaonekana sura zake katika ile tume na itakuwa vyema kama tume ile itatoa taswira ya Kilifi Kaunti watu kutoka katika magatuzi yote madogo saba ya Kilifi ili kuondoa ile tetesi kuwa maeneo mengine hayawezi kupata nafasi ya kuajiriwa katika Kaunti hii.

Nitamvulia kofia Gavana kwa juhudi zake za kuendeleza afya. Amefanya kazi nzuri na mimi kama mwanakamati ya Kamati ya Afya nadhibitishe hilo. Bado tuna mengi ambayo yanastahili kufanywa. Hii ni Wizara inayopewa pesa nyingi sana na utendaji kazi wake sio kwamba ni mbaya lakini bidhaa zake zinaenda kwa haraka sana hivyo kuna uhitaji wa kuwa makini sana, kwa sababu, leo tukisema kuwa tulisambaza madawa katika hospitali zote za Kilifi

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kaunti kutakuwa tunadanganya kwa kuwa kwa sasa hospitali nyingi hazina dawa. Ukizingatia zahanati nyingi sana na kwa kutoa mfano kule kwangu Bamba ya Rimarapera. Juzi nilikuwa nyanjani na nikapewa hizo lalama kwamba hizo zahanati hazina dawa. Nilipouliza muuguzi mkuu alisema dawa ziliisha tangu mwaka jana mwezi wa saba.

Tumekaa muda mrefu na hivyo basi juhudi zile nzuri ambazo Gavana anafanya zitaweza kuregeshwa nyuma ikiwa hatutaweza kuangalia ama wale wamepewa nafasi ya kuangalia mambo kama haya. Nakumbuka ni juzi tukienda pale hospitali kuu ya Kilifi tuliweza kuzindua kitengo ambacho kinasimamia dawa. Hizi zote ni juhudi ambazo mtsahiki amefanya ila bado imebaki katika mikono ya wafanyikazi wa Kilifi kwa hivyo tuombe tu kwamba kila walichotaka tuliweza kuwapatia kama Bunge. Pesa tuliwapatia katika bajeti na wakaomba magari ya kusambaza dawa tukawapa kama Bunge. Lakini ni jambo la kushangaza ikiwa tutafika nyanjani na tuambiwe hakuna dawa. Gari lile la kusambaza dawa sidhani kama liliwahi toka Kilifi na likasambaza dawa mahali popote. Itakuwa ni juhudi za kumregesha nyuma Mstahiki Gavana katika kitengo hiki cha afya na yeye amekivulia kofia kuona ya kwamba wana Kilifi wanakuwa na afya njema.

Pia, nimuombe Mstahiki Gavana tayari tuko na hospitali kuu ambazo zinawakilishwa katika magatuzi yote madogo saba. Kabla tuangalie nani muhimu sana tujenge hospital nyengine lakini zile tulizo nazo kwa sasa tuweze kuziweka vyema ili ziweze kutoa huduma ambazo zinastahili. Nikitoa mfano ya Bamba Sub-County Hospital, imekuwa hivyo kwa miaka mingi sana lakini leo hii ukienda pale zile huduma zinazotolewa ni sawa na huduma za *Health Centre*. Wafanyikazi hawatoshi na majengo hakuna lakini nimshukuru Gavana kwa sababu tumeshikana mikono na kuona ya kwamba hospitali ile baada ya mda mfupi ujao itakuwa imeweza kupanda kiwango chengine.

Pia, nimpatie kongole Mstahiki Gavana kulingana na hatua yake ya kuchukua elimu na kuipa kipaumbele. Ni makubwa na ni mengi amefanya katika sekta ya elimu ila bado nimuombe ya kwamba shule zetu za chekechea bado ziko chini mno. Ikiwa itawezekana, iwe hapa ni mahali ambapo tunaweza kuweka mkazo kwa sababu shule nyingi, nikitoa kwa mfano kwa wadi yangu, niko na shule hamsini na nane (58) na kati ya hizo leo nikikutembeza, Bw. Spika, utashangaa kwa sababu zile shule ziko hali ngumu. Kile kiwango ambacho tunapata hapa ikiwa hakitaweza kuzingatiwa vyema na kuongezwa kulingana na kile kiwango ambacho kinabaki, basi shule zile hazitoweza kuwa sawa kwa wakati. Hivyo basi, nimpatie kongole lakini pia niombe Waziri husika tuweza kujizatiti zaidi.

Pia, nimpatie kongole kwa kuweza kufufua hali ya utalii Kaunti ya Kilifi. Tuliweza kushuhudia ile *Kenya Rivera* ikizinduliwa hapa Malindi na ilikuwa ina mpangilio mzuri wa kuweza kuuza utalii hapa kwetu lakini kutoka ile siku izundiliwe mpaka leo sijui ila niwaambie maafisaa husika kwamba waweze kutia bidii na kuchukua maono ya Gavana wayaweke mbele ili yaweze kusaidia.

Mtsahiki Gavana yuko na nia nzuri sana na watu wetu kwa kuweza kugeuza Mbegu Fund mpaka Wezesha Fund. Kuna changamoto, Bw. Spika, tumeweza kushuhudia kwamba pesa zimetoka, zimewekwa kwa benki ili benki ziweze kupeana mikopo lakini mama zetu kupitia makundi ambayo yapo Kilifi hii hawajaweza kupata hizi pesa kwa urahisi. Nikipeana mfano, juzi nimeweza kumtumia Gavana mwenyewe orodha ya zaidi ya vikundi ishirini na moja (21) ambavyo vimeweza kujizatiti na kufikia mahali inaweza kupata pesa hadi benki yenyewe ikawapatia *notification* kwamba wame-*qualify* na wanaweza kupata pesa. La kushangaza ni kwamba hadi leo hakuna kikundi hata kimoja kimeweza kupata pesa.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Ninashangaa kwamba Wezesha Fund tumeiweka pale ili tuongeze pesa na pesa zinazotolewa zinarudi kwa uharaka lakini hadi leo makundi ya kina mama, vijana na hata walemavu hayajaweza kufaidika na pesa hizi. Benki tulizopewa hizi fedha zimechukulia hizi pesa kama zao. Wameweka masharti mengi ambayo makundi yetu hayawezi kufikia. Ningeomba ya kwamba tuweza kuangalia upya mtazamo huu ili kina mama wetu waweze kupata hizi pesa kwa urahisi. Pesa ziko pale lakini wanaoweza kupata hizi fedha ni mabwenyenye. Wale wanaopewa tenda za Kilifi Kaunti ndio wanaopata hizi pesa. Kina mama wetu ni wachache sana wanaopata. Nikipeana mfano kutoka wadi ya Bamba labda kama nitaambiwa lakini kulingana na ujumbe ambao niko nao, hakuna kundi ambalo limefaidika na hizi pesa. Nina imani sio wadi yangu peke yake; wenzangu wapo wanaweza ongea lakini ipo haja ya kufikiria upya na kuangalia ni vipi hizi pesa zitafaidisha wakaazi wa Kilifi kupitia kwa makundi. Kwa sasa, pesa zipo na zimekwama na wanaofaidikia sitosita kusema ni wale wale mabwenyenye walikuwa wanaendeleza biashara za Kilifi.

Lengine nimpatie kongole Mstahiki Gavana kwa kitengo cha barabara ambacho katika hotuba yake alitueleza mema kwamba ameweza kupiga hatua kwa kutengeza barabara vyema. Nipeane wasi wasi wangu. Hapa Bungeni sisi hupitisha bajeti. Bajeti inayopitishwa huwa kuna kitengo waingereza huita *maintenance kitty*. Hupita takriban zaidi ya shilingi milioni themanini hapa. La kushangaza ni kwamba *kitty* hii haiendi kwa usawa. Nikiongea kwa niaba ya Wadi ya Bamba nitasema sijaona barabara ambayo imefanyiwa *maintenance* na pesa kama hizi na tunamaliza mwaka wa pili, Mheshimiwa Spika. Iko hapa kwa Bunge hili kuweza kupewa Ripoti ya utaratibu kuwa ni vipi pesa hizi ziliweza kutumika kwa kipindi cha miaka miwili. Ni pesa nyingi lakini hazijaweza kufaidi wadi zote. Nikipeana mfano wa wadi yangu hakuna barabara imefanyiwa *maintenance* hata moja na hizi pesa zinafaa kufanyiwa ukarabati wa barabara ambazo zimefunguliwa. Ikiwa zile zilizofunguliwa zitafungana mpaka tuje tufungue tena itakuwa hii *maintenance* ni ya nini? Kwa hivyo, ninampatia kongole mstahiki kwa kitengo hichi lakini wale maofisa ambao wanastahili kufanya hii kazi waweze kuangalia hii Kilifi Kaunti kwa upana na sio kwa marefu vile wanaiangalia.

Pia, niweze kumpa kongole mstahiki Gavana kwa Kitengo cha Ardhi. Amefanya mema na bado anaendelea lakini nimkumbushe ya kwamba bado ardhi ama wananchi wengi wa Kilifi wanaishi kama *squatter*. Ipo haja na umuhimu wa kuweza kuwatoa katika jinamizi hili la *squatter* na kuwapatia ardhi. Saa hii tukiwa tu hapa Bungeni, mheshimiwa Spika, nimeona *clip* ambayo inazunguka ya mheshimiwa Tete na mheshimiwa Brown na mstahiki Gavana mwenyewe wakitetea wakaazi ambao wamepewa *eviction notice* na *police*. Hiyo yote ni kwa sababu ardhi nyingi Kaunti ya Kilifi bado haina hati miliki.

Hivyo basi, yeye akiwa mmoja katika wale waliofanya kazi katika Idara ya Ardhi ana ujuzi na uwezo wa kujua ni vipi anaweza tukwamuwa katika hali hii. Nikirudi kwangu Bamba, kuna *adjudication* ambayo imefanywa toka wakati wa Mstahiki Gavana Kingi mpaka sasa na haijaweza kumaliziwa. Bamba imezungukwa na *ranches* karibu tano ila tunashukuru moja iliweza kusaidika na ikajikwamua kutoka katika kundi la *ranch.* Saa hii tumebaki na *ranches* nne, kulingana na maono na utendakazi wa mstahiki Gavana ni maombi kwamba *ranches* zile kwa sababu hata katika Katiba ya Kenya *ranches* kwa sasa hazitambuliki, tuweze kuzitoa na tuzivunje.

Mimi nimejitolea mwaka huu wa kifedha nitavunja mbili lakini yeye pia aweze kutusaidia ili tuweze kuvunja zile *ranches* na tuweze kukabidhi ardhi hii kwa wananchi. Hiyo itasaidia hata kupunguza zile shida ambazo tuko nazo kwa sasa. Tukiangalia Bamba

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

imezungukwa na watu ambao wanakuja kunyanyasa wananchi wa Bamba. Wao wanajiita wafugaji lakini wanaingia kule waweze kuchukua ardhi kubwa kwa malipo kidogo kwa wananchi lakini serikali ipo ya kaunti ila waliowachiwa katika *management* hizi zote ni *administration* Ngao na utapata hatuna hatua yoyote ambayo sisi kama serikali ya Gatuzi la Kilifi tunaendelea.

Hivyo basi, ningependa kumpongeza mstahiki lakini pia aniambie maofisaa ambao wanashughulikia hii kwamba waweze kujizatiti na kuona ya kwamba ardhi ya Kilifi inaregeshwa na kupewa hatimiliki kwa wananchi wa Kilifi. Nimpatie kongole mstahiki Gavana kwa kazi nzuri anayosifanya kupitia katika hali ya kuwezesha wananchi. Kwa mfano, akiwa na mradi wa inua jamii ambao juzi ama kwa sasa unaendelea, kuna wazee na mayatima ambao wanaweza kuwekwa katika mradi ili waweze kufaidika. Hapo nimpe kongole sana na nimwambie azidi kufikiria na idadi ile izidi kuongezeka kadri ya miaka tunavyoendelea.

Pia, nimpatie kongole mstahiki Gavana katika hotuba yake kwa Kitengo cha Ukulima. Ni mengi mema ameweza kuyafanya na mengi ambayo ananuia kuyafanya ambayo yataweza kuinua Kilifi na kuweza kuweka wana Kilifi mahali ambapo kiukweli Mwenyezi Mungu akiendelea kuturuzuku mvua vile inaendelea baada ya miaka mitatu hautowahi sikia njaa tena huku kwetu. Kile kinastaajabisha katika sekta hii ni kwamba *tractors* zetu zote hazifanyi kazi. Wakati wa msimu wa mvua umefika na ukipiga simu kwa wizara husika wanakuambia *tractors* zote zimelala. Kwa hivyo, ni jambo la kuhuzunisha na tunawapatia kama changamoto ya kwamba zile *tractors* ambazo zimelala ziweze kufufuliwa ili ziweze kusaidia wananchi katika hali yao ya ukulima ndio tuweze kupata….

The Speaker (Hon. Mwambire): Zinaitwa tinga tinga sio *tractor* kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Kwa sababu wale wahenga kule Bamba wanaweza kukosa kukuelewa kile unachoongea.

Hon. Mohamed: Asante, Bw. Spika. Haya, yale matingatinga ya kulima. Haya ni mambo ambayo ni muhimu sana na ikiwa itaweza kuzingatiwa, basi tuweze kusaidika ili tuweze kupata chakula cha kutosha. Unajua, mheshimiwa Spika, serikali hii ya mstahiki Gavana Mung'aro iliingia na bahati sana. Kule nyuma mstahiki Gavana Kingi alikaa miaka zaidi ya sita hakuweza kupata mvua na kwa hivyo basi alikuwa anagawanya chakula cha msaada kila siku lakini serikali hii ya Gavana Mung'aro kuingia tu ikapata mvua hadi leo kunanyesha mvua. Hivyo basi chakula cha msaada kidogo kimeweza kupungua na wananchi wameweza kujitayarishia chakula chao mashambani.

Mimi nikikupatia mfano siku hizi nalala kule Bamba maanake wakati nikipata hiki kiti nilisema kama hivi ndivyo ilivyo; sidhani kama nitaweza kumaliza miaka mitano maanake ilikuwa kila siku pale nyumbani sikosi watu chini ya mia mbili. Wote wamekuja kwa sababu ya njaa, lakini siku hizi naweza lala niamke asubihi niende shamba na sina mtu kwa sababu kila mmoja yuko shambani na chakula kipo kwa hivyo hapa tunaweza kumshukuru mstahiki kwa sababu aliweza kugawanya Mbegu kwa wakati unaofaa na watu wakaweza kusaidika. Kwa hivyo, tunamshukuru sana.

Ninukuu kwa lugha ya kimombo, najua mstahiki Spika, hii lugha ni yetu lakini huwa kama vile Seneta alivyosema huwa ni ngumu kidogo. Kitengo cha KEMFED *(Kenya Marine Fisheries and Socio-Economic Development)* hichi ni kitengo ambacho kinasaidia. Lakini tukiangalia *phase one* yake ama roundi ya kwanza na roundi ya pili, sio Wadi zote ziliweza kuguswa. Hivyo basi, tupeane changmoto ya kwamba japo tunajua inagusa sana wadi ambazo ziko karibu na bahari lakini kuna ile miradi ambayo inaweza kusaidia kwa mfano ufugaji wa

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mbuzi kuweza kusaidia jamii kama vile kujenga hospitali na kujenga mashule. Hii ni miradi ambayo inaweza kupelekwa hata zile wadi nyingine ambazo ziko mbali na bahari kwa mfano Bamba.

Bamba iko mbali na bahari lakini ukiwajengea shule watajua KEMFED ilifika; ukiwapatia ufugaji wa ng'ombe ama mbuzi ndio utakuja kujua kwamba Bamba kuna mbuzi tamu. Maanake tutazilea vizuri na ukifika itakuwa vyema. Kwa hivyo, hapa pia watie kongole kwa sababu wana ushirikiano mwema na vitengo hivi ila viweze kupeana kwa usawa.

Mwisho kabisa mstahiki Gavana anafanya jambo jema sana kwa sababu yeye wakati akiingia hata katika maono yake maji, afya na kilimo yako katika kipao mbele. Tukiangalia vile anafanya kazi kwa sekta ya maji anafanya vyema lakini bado kuna mambo ambayo tunastahili kuyafanya. Yako mambo ambayo yanastahili kuwa yachunguzwe na yaangaliwe kwa ukaribu. Kwa mfano, mstahiki Gavana anaweza kupeena miradi mikubwa sana ya maji na sio kwamba kule nyanjani hakuna *lines* za maji ama hakuna maji. Maji yapo lakini kuna changamoto ndogo ndogo ambazo zinafaa kuangaliwa kwa ukaribu ili mambo kama yale yakitatuliwa maji yatakuwa yanaweza kupatikana kwa mkaazi wakati wowote na saa yeyote. Lakini utakuta ya kwamba mambo hayo hayajaangaliwa kwa ukaribu.

Nikikupa mfano, kule Bamba ni eneo ambalo leo hii mvua ikiacha na ukinipatia miezi mitano au sita, utasikia ukame wa maji Bamba umerudi. Na sio kwamba ati hakuna mabomba ya maji; mabomba ya maji yapo lakini kuna utepetevu ambao huwa unafanyika. Kwa mfano, kwa sasa kuna *transformer* pale Mulungu wa Mawe ambayo inafaa kupeana umeme wa kusambaza maji. Tangu tuingie katika serikali hii, mimi na Gavana tumekuwa na ukaribu wa kuangalia ule mtambo lakini utashangaa baada ya mwezi unaambiwa *transformer* iliwekwa na ikafanya kazi siku mbili ikapasuka tena. Sasa utapata lile bomba lililowekwa na serikali iliyopita na kuzinduliwa rasmi na Gavana wakati ameingia la Ganze hadi Jira, kule kwao wanaona bomba tu lakini halina maji.

Watu wa maji wanasema lazima maji yasambazwe siku tatu mfululizo ndio yaweze kufika Jira. Mara nyingi wanatumia mafuta *generator* na mafuta ya *petrol*; sasa *generator* haiwezi kupiga maji mfululizo kwa siku tatu. Inapiga kwa masaa tu. Kwa hiyo inamaanisha ikiwa hakutakuwa na ukarabati wa kwamba umeme upatikane pale basi shida ya maji Bamba itabaki pale tu.

Shida ndogo ndogo ambazo ninataka kuwaambia wahusika kwamba afadhali tuwekeze katika kuboresha miundo misingi yetu ili kusaidia wananchi wetu.

Hotuba ya Gavana ilikuwa ya kusisimua, ilituonyesha kuwa ana utendakazi wema ndani ya kaunti. Kwa hayo, shukurani kwa nafasi hii.

The Speaker (Hon. Mwambire): Asante sana umetupa lugha tofauti umesema Bamba mnalea mbuzi hamfugi. Sasa mheshimiwa Twaher ataangalia kwa kamusi kama mbuzi inalelewa ama hufugwa kwa Kiswahili sanifu. Asante sana kwa changizo zako.

Waheshimiwa, huwa ninapeana fursa kwa walioomba nafasi ya kuongea kwa hiyo kama hujaongea kuhusu hotuba ya Gavana tafahhali huu ndio wakati maana leo ndio siku ya mwisho kutoa changizo zetu kuhusu swala hilo.

Kama hakuna changizo zozote kuhusiana na hotuba ya Gavana aliyotowa tarehe 13 mwezi wa tatu mwaka huu, nataka kuchukua fursa hii kuwashukuru wale ambao walitoa changizo zao na hizo zote zitafikishwa upande wa serikali. Kuna Kamati mbali mbali zilizogusiwa katika hotuba ya Gavana; hizo zinaweza fwatilizia. Kuna baadhi ya miradi iliyokuwa na matatizo wanaweza kufwatiliza upande huo na walete Ripoti Bungeni kwa

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mukhtasari yaliyotendeka katika serikali yake. Katika Kamati zenu mnaweza fwatilia yaliyogusiwa na kuhakikisha kila kitu kiko sawa ili wakaazi wa Kilifi wapate huduma bora. Tuangalie utandaji kazi kwa manufaa ya wana Kilifi. Kwa sasa, tunafunga changizo kuhusu hotuba ya Gavana.

ADJOURNMENT

The Speaker (Hon. Mwambire): Kwa sababu hakuna lingine la kushughulikiwa kwa sasa, Bunge hili limefungwa hadi kesho saa tatu asubuhi. Muwe na jioni njema.

The House rose at 3:20 p.m.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*